



Karibu kwa Idara ya Dharura ya Hospitali ya Watoto ya Perth

Tupo hapa kumsaidia mtoto wako kupata huduma anayohitaji.

Tunatunza watoto wa umri wa miaka 15 au chini mwenye dharura za kimatibabu au ayfa ya akili. Ni bure kwa waraia au wakazi wa Australia.

Hospitali ya Watoto ya Perth inaitwa pia PCH. Idara ya Dharura (Emergency Department) inaitwa pia ED.



Huduma ya Mkalimani

Omba kwa mkalimani kama huelewi au kukusaidia kuongea na sisi. Huduma hiyo ni bure.

Muda wa kusubiri

Inaweza kuwa na shughuli nyingi katika Idara ya Dharura pamoja na watoto wagonjwa wengi wanaosuburi kuangaliwa. Watoto wagonjwa zaidi wanaangaliwa kwanza. Utaratibu na nyakati za kusubiri ni sawa kama utafika kwa gari la wagonjwa.

Tafadhali utuambie kama ukipanga kuondoka kabla ya hatujatiba mtoto wako.

Nini kinatokea katika Idara ya Dharura



Triage

Triage husaidia wafanyakazi kuamua mtoto wako anahitaji kuangaliwa na daktari kwa haraka kiasi gani. Wataangalia mtoto wako na kukuuliza maswali.



Subiri kuonekana na daktari

Utaenda ndani Idara ya Dharura kusubiri kwa muuguzi au daktari kumwona mtoto wako. Karani atauliza maswali wakati unaposubiri.



Kuonekana na muuguzi au daktari

Watauliza maswali na kumchunguza mtoto wako kusaidia kuelewa kile ambacho ni tatizo.



Ongea na muuguzi au daktari wako

Daktari au muuguzi ataeleza kile ambacho ni tatizo na kile mtoto wako anachohitaji. Utulize maswala kwa wakati wowote.



Vipimo au matibabu


Mtoto wako anaweza kuhitaji kipimo cha damu, eksrai, au vipimo vingine ili kujua ni nini ni shida. Anaweza pia kupokea tiba wakati yupo kwenye ED. Labda atahitaji kusubiri wakati huu.



Subiri kuondoka au kuuu kwa matibabu zaidi

Daktari wako anaweza kuhitaji kumtunza mtoto wako ili kuhakikisha kuwa halizidi kuwa mbaya au kuona majibu yake kwa matibabu. Utapata mafunzo yoyote kabla kuondoka. Ikiwa mtoto wako anahitaji kukaa kwa tiba zaidi, atahamishiwa katika chumba kingine hospitalini.

Kutana na timu yako ya huduma ya afya: kuna watu wengi wanaosaidia kumtunza mtoto wako



Ikiwa unafikiri mtoto wako anajisikia maumivu

Tafadhali ongea na muuguzi atakayepima mtoto wako na kupanga tiba inayofaa kupunguza maumivu.

Je, unahangaika? Tunahitaji kujua.



Ikiwa mtoto wako anaonekana kuugua zaidi au ana tabia isiyo ya kawaida, tuambie mara moja. Unamjua mtoto wako vizuri zaidi. Tutakusikiliza.

Ikiwa Kiingereza chako ni chache sema 'Emergency Waiting Room' or just your room number (au nambari ya chumba chako tu).

Kwenda nyumbani

Wakati mtoto wako anapokuwa tayari kwenda nyumbani, daktari au muuguzi atakupa maelezo kadhaa juu ya unachohitaji kufanya ili kumtunza mtoto wako. Tafadhali utuulize kwetu maswali yoyote unayokuwa nayo. Tunaweza pia kukupa barua kwa daktari wako wa mtaani.

Wakati upo nyumbani

Fuata mafunzo yoyote uliyopewa na daktari. Ikiwa unahangaika kuwa mtoto wako hajaanza kuponya, unaweza:

- kumtembelea daktari wako wa mtaani;
- piga simu kwa Health Direct kwenye 1800 022 222; au
- tembelea Kliniki ya Huduma ya Dharura ya GP.

Ikiwa ni dharura, piga simu kwa 000 kwa ambulensi au rudi kwa Idara ya Dhurura.

Pata maelezo zaidi kuhusu muda wako katika PCH

Tembelea tovuti yetu kwa pch.health.wa.gov.au au mwulize mfanyakazi au mjitoleaji juu ya:



- kusimamisha gari (kumbuka kusogeza gari lako kutoka eneo la 'kushuka haraka' kwenda eneo la kusimamisha magari)
- vyoo, vifaa vya kupatikana, vifaa vya wazazi na meza za kubadlisha nepi
- chakula na vinywaji
- maoni, pongezi na malalamiko
- Wi-Fi ya bure ya PCH (mtandao wa HEALTH-Guest, haina haja ya neno la siri).